



HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA

Unapojibu tafadhali taja

Kumb. Na. KGR/ML/HW/A.225/VOL.V/27

Tarehe: 26/06/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA TAREHE 26 JUNI 2023

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba anawatangazia nafasi za kazi ya muda watanzania wote wenye sifa na nia ya kuajiriwa katika nafasi ya Wakusanya Mapato.

WAKUSANYA MAPATO – NAFASI 30

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe na mafunzo ya Taaluma yoyote katika ngazi ya Cheti/Astahhada. Wenye fani ya Uhasibu, Biashara, au Kodi watapewa kipaumbele.
2. Awe na uwezo wa kutumia Kompyuta au Simu janja.
3. Awe na wadhamini wawili (2) ambao ni watumishi wa Umma
4. Mwombaji aambatanishe, kitambulisho cha Taifa (NIDA), au Namba ya NIDA.
5. Mwombaji aambatanishe barua za wadhamini ambao ni watumishi wa Umma.

KAZI/MAJUKUMU

1. Kukusanya mapato ya Halmashauri kwa usahihi kwa mujibu wa Sheria ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Muleba.
2. Kukusanya Mapato ya Halmashauri kwa njia ya mashine ya kukusanyia mapato yaani PoS.
3. Kuwasilisha benki kiasi cha fedha kinachokusanywa kila siku.

MALIPO YA MSHAHARA KWA WATAKAOAJIRIWA

Malipo yatakuwa sh. 6,000 kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi.

VIGEZO NA MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 – 45
2. Mwombaji awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la jinai.
3. Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya taaluma nakala ya cheti cha Kidato cha nne au cha sita vilivyothibitishwa na Hakimu au Wakili anayetambulika na Serikali.
4. Mwombaji aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
5. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed Curriculum Vitae) ikiwa na anuani, namba za simu za kuaminika, pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu (3) na picha mbili za “passport size” za hivi karibuni (ziandikwe jina kwa nyuma).
6. Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati za matokeo za kidato cha nne na sita (Form IV and VI Results Slips) na Transcript ambayo haikuambatanishwa na cheti havitakubaliwa.
7. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (NECTA au NACTE).
8. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma kwa sababu yoyote ile hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.
9. Waombaji watakaowasilishaji vyeti, taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria na mamlaka zinazohusika.
10. Maombi yote yaandikwe kwa mkono.

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Muleba,
S.L.P. 131,
MULEBA.

Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni siku ya Jumanne, tarehe 09 Julai 2023, saa 09:30 Alasiri.


Christina P. Akyoo,

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI.



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya S.L.P 131 Muleba, Kagera Barua Pepe:
ded@muleba.go.tz Simu +255 28 2224013 Fax +255 28 2224168